



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA KILIMO**  
**TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA**  
**TANZANIA**



Dodoma, 30/01/2022

**TAARIFA KWA UMMA**

**VYAMA VYA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO (SACCOS),  
VYATAKIWA KUFUNGA HESABU KWA MWAKA WA FEDHA  
UNAOISHIA DESEMBA 31, 2021**

**M**waka wa Fedha wa Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) unaanzia Mwezi Januari 1 na kuisha Mwezi Desemba 31 kila mwaka. Mara baada ya kupita kwa muda huo, Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt. Benson Ndiege, amezitaka na kuzielekeza SACCOS zote kuhakikisha zimefunga Hesabu zake za Mwaka husika kwa kuzingatia matakwa ya kifungu cha 55(2) cha Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya Mwaka 2013 na kanuni ya 55 ya Kanuni za Vyama vya Ushirika za Mwaka 2015.

Aidha, Mrajis amezielekeza SACCOS kuzingatia Kifungu cha 40(1) cha Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha Na.10 ya Mwaka 2018 na Kanuni ya 59 ya Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha (SACCOS) za Mwaka 2019 na kuzitaka SACCOS zote kuwasilisha Taarifa za Fedha kwa Mkaguzi wa Nje (Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika - COASCO).

Katika kutekeleza matakwa haya ya Sheria na Kanuni, Mrajis amewaelekeza Viongozi na watendaji wa SACCOS nchini kuhakikisha wanafunga Hesabu za Mwaka 2021 mapema na kuziwasilisha kwa Wakaguzi wa Nje ndani ya Mwezi wa Februari 2022, ili hesabu hizo ziweze kukaguliwa na kurudishwa kwao mapema. Pia, ameelekeza kuwa utaratibu huu utapaswa kuzingatiwa na viongozi na watendaji wote wa SACCOS kila Mwaka.

Aidha, Viongozi wa SACCOS wanapaswa kujibu hoja zote zilizotolewa na zitakazotolewa na Wakaguzi ili kuondokana na uwepo wa Hati zisizoridhisha pamoja na Hati Chafu. Chama kitakachoshindwa kujibu hoja husika na kupata Hati Chafu, Viongozi na Watendaji wake watapaswa kuwajibika kwa kuzingatia matakwa ya Kifungu cha 55(13) cha Sheria ya Vyama vya Ushirika, kanuni ya 85(g) ya Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha (SACCOS) za Mwaka 2019.

Ofisi ya Mrajis katika ngazi ya Taifa, Mikoa na Halmashauri zote zitafuatilia utekelezaji wa maelekezo haya kwa karibu na kuchukua hatua stahiki kwa wote watakaobainika kwenda kinyume na maelekezo haya na kushindwa kutekeleza matakwa ya Sheria na Kanuni zake kama zinavyoelekeza.

Aidha, ofisi inaendelea kutahadharisha umma na SACCOS zisizo na Leseni kutoendelea kufanya biashara ya huduma ndogo za fedha pasipokuwa na Leseni husika, kwani ni kwenda kinyume na matakwa ya Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha Na.10 ya Mwaka 2018, Kifungu cha 16. Ni matarajio ya ofisi kuwa kila SACCOS itatekeleza maelekezo haya pamoja na matakwa ya Sheria na Kanuni zake ili kuepuka adhabu na hatua zinazoweza kuchukuliwa na ofisi kwa kukiuka matakwa ya Sheria hiyo.

Imetolewa na:

Kitengo cha Habari na Mawasiliano  
**Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC)**